Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project

Published on *Books on Islam and Muslims* | *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Zama Zitakazofika

Authors(s):

Amiraly M.H. Datoo [3]

Zama Zitakazofika

Makala haya yametarjumiwa na kushereheshwa na:
Amiraly M.H. Datoo (*PO Box 838 Bukoba, Tanzania*)

Hadithi hii ilisomwa na: Sheikh Akmal Hussein Taheri – Bukoba.

Amesema Mtume sa.w.w. kuwa: Utafika wakati katika Ummah wangu ambapo:

1. Nyuso za watu zitakuwa za kibinadamu lakini nyoyo zao zitakuwa za kishetani na mfano wao utakuwa kama mnyama mwenye kudhuru na ambaye daima hutaka damu tu

2. Kamwe hawazuii watu kutotenda maovu bali wao wenyewe watakuwa wakiyatenda hayo hayo

3. Iwapo watu kama hao watafuatwa basi watawatumbukiza watu katika hali ya mashaka

4. Iwapo utaongea nao, basi daima watakukadhibisha

5. Na iwapo utajaribu kujitenga nao basi wataanza kukusengenya

6. Kwao Sunnah ni bida'a na bida'a kwao ni Sunnah mifano ni mingi kama hii ya Mi'raji, uzawa wa Mtume sa.w.w. , n.k.

7. Watu walio na heshima kwao ndio wanachukuliwa kuwa waovu

8. Na wale walio waovu miongoni mwa watu ndio wanaoheshimiwa na kutukuzwa

9. Waumini miongoni mwao ni watu waliokandamizwa

10. Ambapo waovu ndio wanaotukuzwa kwao

11. Watoto wao hawana heshima wala tabia njema

12. Na wake zao watakuwa waovu kiasi kwamba waume zao watakuwa wamewachoka wake zao na watajaribu kujiepusha nao. (Wanawake kutovaa hijabu na mavazi ya heshima yenye kuwasitiri wao, kujipamba na kujirembesha kwa ajili ya wengine, kupeana mikono na wanaume wasio waume zao. Ama wanaume pia hawapo nyuma katika masuala kama haya kwani utayasikia kuwa wanaume wengine wanao wake wa pembeni hata bila ndoa, vile vile utawasikia wauza pombe kuwa biashara yao inaanguka katika mwezi mtukufu wa Ramadhani ati wanywaji wa pombe wengi ni Waislamu

13. Maulamaa wao hawawaongozi kwa mema na wala hawawakatazi dhidi ya maovu yaliyo miongoni mwa Waumini (ati kwa sababu za fedha na hofu ya maslahi yao kwamba yeye hujiinamisha mbele ya matajiri na kuwadhalilisha masikini

14. Kuomba msaada wao ni kujidhalilisha

15. Na kwa kuwaomba msaada wakati wa shida, basi huwadharau waombaji

16. Na kuomba chochote kutoka kwa watu kama hawa ni umasikini na ufukara

17. Na utakapofika wakati kama huo, basi Allah swt hatawanyeshea mvua hata kwa tone moja wakati utakapofika msimu wa mvua na badala yake kutakuwapo na mvua pasi na msimu wake. Sasa jee mvua zisizo za msimu zinasaidia vipi ? Jee hii si dalili ya adhabu na maafa ?

18. Na watu watasalitiwa na wadhalimu waovu kabisa

19. Ili watu hao watawapeleka watu kuelekea makali ya adhabu

20. Nyakati hizo watu wataomba dua lakini hazitakubaliwa

21. Nyuso za watu zitakuwa za kibinadamu lakini nyoyo zao zitakuwa za kishetani na mfano wao utakuwa kama mnyama mwenye kudhuru na ambaye daima hutaka damu tu

22. Kamwe hawazuii watu kutotenda maovu bali wao wenyewe watakuwa wakiyatenda hayo hayo

23. Iwapo watu kama hao watafuatwa basi watawatumbukiza watu katika hali ya mashaka

24. Iwapo utaongea nao, basi daima watakukadhibisha

25. Na iwapo utajaribu kujitenga nao basi wataanza kukusengenya

26. Kwao Sunnah ni bida'a na bida'a kwao ni Sunnah mifano ni mingi kama hii ya Mi'raji, uzawa wa

Mtume sa.w.w., n.k.

27. Watu walio na heshima kwao ndio wanachukuliwa kuwa waovu

28. Na wale walio waovu miongoni mwa watu ndio wanaoheshimiwa na kutukuzwa

29. Waumini miongoni mwao ni watu waliokandamizwa

30. Ambapo waovu ndio wanaotukuzwa kwao

31. Watoto wao hawana heshima wala tabia njema

32. Na wake zao watakuwa waovu kiasi kwamba waume zao watakuwa wamewachoka wake zao na watajaribu kujiepusha nao. (Wanawake kutovaa hijabu na mavazi ya heshima yenye kuwasitiri wao, kujipamba na kujirembesha kwa ajili ya wengine, kupeana mikono na wanaume wasio waume zao. Ama wanaume pia hawapo nyuma katika masuala kama haya kwani utayasikia kuwa wanaume wengine wanao wake wa pembeni hata bila ndoa, vile vile utawasikia wauza pombe kuwa biashara yao inaanguka katika mwezi mtukufu wa Ramadhani ati wanywaji wa pombe wengi ni Waislamu

33. Maulamaa wao hawawaongozi kwa mema na wala hawawakatazi dhidi ya maovu yaliyo miongoni mwa Waumini (ati kwa sababu za fedha na hofu ya maslahi yao kwamba yeye hujiinamisha mbele ya matajiri na kuwadhalilisha masikini

34. Kuomba msaada wao ni kujidhalilisha

35. Na kwa kuwaomba msaada wakati wa shida, basi huwadharau waombaji

36. Na kuomba chochote kutoka kwa watu kama hawa ni umasikini na ufukara

37. Na utakapofika wakati kama huo, basi Allah swt hatawanyeshea mvua hata kwa tone moja wakati utakapofika msimu wa mvua na badala yake kutakuwapo na mvua pasi na msimu wake. Sasa jee mvua zisizo za msimu zinasaidia vipi ? Jee hii si dalili ya adhabu na maafa ?

38. Na watu watasalitiwa na wadhalimu waovu kabisa

39. Ili watu hao watawapeleka watu kuelekea makali ya adhabu

40. Nyakati hizo watu wataomba dua lakini hazitakubaliwa.

Category:

General [4]

Source URL: https://www.al-islam.org/node/24932

Links

[1] https://www.al-islam.org/user/login?destination=node/24932%23comment-form

[2] https://www.al-islam.org/user/register?destination=node/24932%23comment-form

[3] https://www.al-islam.org/person/amiraly-mh-datoo

[4] https://www.al-islam.org/library/general-belief-creed